



TANGAZO KWA UMMA

BENKI KUU YA TANZANIA YAONGEZA MUDA WA USIMAMIZI WA BANK M TANZANIA PLC

Itakumbukwa kwamba, kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha sheria namba 56(1)(g)(iii) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania iliamua kuchukua usimamizi wa Bank M Tanzania Plc (Bank M) kuanzia tarehe 2 Agosti 2018 baada ya kubaini kuwa Bank M ilikuwa na upungufu mkubwa wa ukwasi kinyume na matakwa ya sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake.

Baada ya kuchukua usimamizi wa benki hii, Benki Kuu ya Tanzania ilisitisha shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za Bank M kwa muda wa siku tisini ili kuipa nafasi Benki Kuu ya Tanzania kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi wa suala hili. Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuarifu umma kuwa mchakato wa kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi wa matatizo ya Bank M haujakamilika hivyo muda wa usimamizi umeongezwa kwa kipindi cha siku sitini kuanzia tarehe 2 Novemba 2018.

Benki Kuu ya Tanzania inauhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika mabenki kwa lengo la kuleta ustahimilivu katika sekta ya fedha.

BENKI KUU YA TANZANIA

7 Novemba, 2018